Tafuta Kekima Kwa Bidii

na

Ellis P. Forsman

Tafuta Kekima Kwa Bidii

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 11, 2011

Tafuta Hekima Kwa Bidii

Mith. 2:1-22

Kusudi la kuwa na hekima

Katika sura ya kwanza ya Mithali, tunaona kusudi la kitabu.

Mith. 1:1-6, "*Mithali za Sulemani mwana wa Daudi, mfalme wa Israeli. Kujua hekina na adabu; kutambua maneno ya ufahamu; kufundishwa matendo ya busara, katika haki na hukumu ya adili. Kuwapa wajinga werervu, na kijana maarifa na hadhari; mwenye hekima asikie na kuongezewa elimu, na mwenye ufahamu ayafikie mashauri yenye njia. Kufahamu mithali na kitendawili, na maneno ya wenye hekima na mafumbo yao.*"

Wazo la Mithali, jinsi utii wa Mungu ulivyo chanzo cha maarifa. Mith. 1:7, "*Kumcha BWANA ni chanzo cha maatifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu.*"

Faida ya kuwa sikiliza wazazi. Mith. 1:8-9, "*Mwanangu yasikilize mafundisho ya baba yako, wala usiiache sheria ya mama yako, kwa maana hayo yatakuwa kilemba cha neema kichwani pako, na mikufu shingoni mwako.*"

Hatari ya marafiki waovu. Mith. 1:10-19, "*mwanangu mwenye dhambi wakikushawishi, wewe usikubali. Wakisema, haya, njoo pamoja nasi, na tuvizie na kumwaga damu; tumwotee asiye na hatia, bila sababu; tuwameze hai kama kuzimu, na wazima kama wao washukao shimoni. Tutapata mali yote ya thamani, tutazijaza nyumba zetu mateka. Wewe utashirikiana nasi; tutakuwa na vitu vyote shirika. Mwanangu usiende njiani pamoja nao; uzuie mguu wako usiende katika mapito yao. Maana miguu yao huenda mbio maovuni, nao hufanya haraka ili kumwaga damu. Kwa kuwa mtego hutegwa bure, mbele ya macho ya ndege ye yote. Na hao hujiotea damu yao wenyewe, hujinyemelea nafsi zao wenyewe. Ndivyo zilivyo njia za kila mwenye tama ya mali; huuondoa uhai wao walio nayo.*"

Umuhimu wa kusikiliza hekima wakati kunapo nafasi. Mith. 1:20-33, "*Hekima hupaza sauti yake katika njia kuu, hutoa sauti yake katika viwanja; hulia penye mikutano mikubwa ya watu, mahali pa kuyaingilia malango, nadani ya mji hutamka maneno yake. Enyi wajinga hata lini mtapenda ujinga? Na wenye dharau kupenda dharau yao, na wapumbavu kuchukia maarifa? Geukeni kwa ajili ya maonyo yangu;*

tazama nitawamwagia roho yangu, na kuwajulisheni maneno yangu. Kwa kuwa nimeita nanyi mkakataa; nimeunyoosha mkono wangu asiangalie mtu; bali mmebatilisha shauri langu, wala hamkutaka maonyo yangu; mimi nami nitacheka siku ya msiba wenu, nitadhihaki hofu yenu ifikapo; hofu yenu ifikapo kama tufani, na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli, dhiki na taabu zitakapo wafikia. Ndipo watakaponiita, lakini sitaitika; watanitafuta kwa bidii, wasinione. Kwa kuwa walichukia maarifa, wala hawakuchagua kumcha BWANA. Hawakukubali mashauri yangu, wakayadharau maonyo yangu yote. Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, watashiba mashauri yao wenyewe. Maana kurudi nyuma kwao wajinga kutawaua, na kufanikiwa kwao wapumbavu kutawaangamiza. Bali kila asikilizaye atakaa salama, naye atatulia bila kuogopa mabaya."

Faida za kutafuta hekima

Sura ya pili ya Mithali inaelezea faida za kutafuta hekima na maonyo ya kutafuta hekima kwa bidii. Mith. 2:1-4, "*Mwanangu kama ukiyakubali maneno yangu, na kuyaweka akiba maagizo yangu; hata ukatega sikio lako kusikia hekima, ukauelekeza moyo wako upate kufahamu; naam, ukiita busara, na kupaza sauti yako upate ufahamu; ukiutafuta kama fedha, na kuutafutia kama hazina iliyositirika,*"

Na orodha ya faida zitakazotokana na utafutaji huo. Mith. 2:5-22, "*Ndipo utakapofahamu kumcha BWANA, na kupata kumjua Mungu. Kwa kuwa BWANA huwapa watu hekima; kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu; huwawekea wanyofu hakiba ya hekima kamili; yeye ni ngao kwao waendao kwa ukamilifu, apate kuyalinda mapito ya hukumu, na kuhifadhi njia ya watakatifu wake. Ndipo utakapofahamu haki na hukumu, na adili, na kila njia njema. Maana hekima itaingia moyoni mwako, na maarifa yatakupendeza nafsi yako; busara itakulinda; ufahamu utakuhifadhi. Ili kukuokoa na njia ya uovu, na watu wanenao yaliyopotoka; watu waziachao njia za unyofu, ili kuziendea njia za giza; wafurahio kutenda mabaya; wapendezwao na upotoe wa waovu; walipotoka katika njia zao; walio wakaidi katika mapito yao. Ili kuokoa na Malaya, naama Malaya mwenye kubembeleza kwa maneno yake; amwachaye rafiki wa ujana wake, na kulisahau agano la Mungu wake. Maana nyumba yake inaelekea mauti, na mapito yake yanakwenda kwenye wafu. Katika hao wamwendeao harudi hata mmoja, wala hawazifikilii njia za uzima. Ili upate kwenda katika njia za watu wema, na kuyashika mapito ya wenye haki. Maana wanyofu watakaa katika nchi, na wakamilifu watadumu ndani yake. Bali waovu watatengwa na nchi, nao wafanyao hila watang'olewa.*

Faida za kutafuta hekima zinapatika ikiwa tu tukitafuta kwa nia njema.

Sifa za utafutaji sana wa hekima

Kama ilivyoelezwa na Sulemani:

Inahitaji uhiari. Mith. 2:1, "*Mwanangu kama ukiyakubali maneno yangu, na kuyaweka akiba maagizo yangu.*"

- Kukubali neno la Mungu.
- Kuweka hazina(thamani ya hali ya juu na kukumbuka) maagizo ya hekima.

Inahitaji kujihusisha. Mith. 2:2-3, "*Hata ukatega sikio lako kusikia hekima, ukauelekeza moyo wako upate kufahamu; naam, ukiita busara, na kupaza sauti yako upate ufahamu;*"

- Ya masikio (hiari ya kusikia hekima).
- Ya moyo (hiari ya kuelewa).
- Ya mdomo (hiari ya kulia kwa ajili ya kiu na uelewa).

Inahitaji juhudi ya hali ya juu. Mith. 2:4, "*Ukiutafuta kama fedha, na kuutafutia kama hazina hazina iliyositirika;*"

Utafutaji kwa shauri ilo hilo kama kutafuta fedha na hazina zingine zilizofichika. Hivyo utafutaji sana wa hekima inahitaji "vyote nje" nguvu ya upande wetu.

Kama ilivyo kwa Wakristo leo.

Inahitaji kusikiliza neno la Mungu. Mith. 2:2, "*Hata ukatega sikio lako kusikia hekima, ukaelekeza moyo wako upate kufahamu;*"

Kuwasikiliza wahubiri na waalimu kwa makini (kwa utayari wote). Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Inahitaji kusoma Biblia kivyako (kuyachunguza maandiko kila siku). Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekeve wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Inahitaji kutamali katika neno la Mungu. Mith. 2:2, "*Hata ukatega sikio lako kusikia hekima, ukauelekeza moyo wako upate kufahamu;*"

Chukua wakati na kumulika au kufikiria neno. Fil. 4:8, "*Hatimaye ndugu mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya stahaa, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.*"

Kama mtunzi wa Zaburi alivyoimba kutafakari kwake. Zab. 119:97-100, "*Sheria yako naipenda mno ajabu, ndiyo kutafakari kwamba mchana kutwa. Maagizo yako hunitia hekima kuliko adui zangu, kwa maana ninayo sikuzote. Ninazo akili kuliko wakufunzi wangu wote, maana shuhuda zako ndizo nizifikirizo. Ninao ufahamu kuliko wazee, kwa kuwa nimeyashika mausia yako.*"

Inahitaji maombi ya bidii kwa ajili ya hekima. Mith. 2:3, "*Naam, ukiita busara, na kupaza sauti yako upate ufahamu.*"

Tunapaswa kuomba kwa imani. Yak. 1:5, "*Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu wala hakemei; naye atapewa.*"

Lazima tuendelee katika kuomba kwetu. Mat. 7:7-11, "*Ombeni nanyi mtapewa, tafuteni nanyi mtaona, bisheni nanyi mtafunguliwa, kwa maana kila aombaye hupokea, naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Au kuna mtu yupi kwenu ambaye mwanaye akimwomba mkate atampa jiwe? Au akiomba samaki atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je si zaidi sana Baba yenu mbinguni atawapa mema wao wamwombao.*"

Inahitaji juhudi zile zile ambazo wengine wanazitumia katika kutafuta utajiri wa kimwili. Mith. 2:4, "*Ukiutafuta kama fedha, na kuutafutia kama hazina iliyositirika;*"

Katika Kristo vimefichwa hazina zote za hekima na maarifa. Kol. 2:3, "*Ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimefichwa.*"

Hapa kuna jaribio rahisi kuona kama unatumia nguvu sahihi kutafuta hekima: kama ukifanya kazi kwa juhudi kwa ajili ya muajiri wako kama jinsi unavyofanya katika kutafuta hekima ya Mungu, je utakuwa na kazi ako kwa muda mrefu?

Kupata hekima ya Mungu leo inahitaji juhudi zile zile kama ilivyokuwa kwa Sulemani leo. Je juhudi ni bora? Hebu twende katika Mith. 2:5-22 na kuona ni nini…

Faida za kutafuta hekima

Ujuzi wa Mungu na ulinzi wake

Utaelewa kumwogopa Bwana na kupata ujuzi wa Mungu. Uoga huo wa Bwana ambao ndio chanzo cha maarifa.

- Mith. 2:5, "*Ndipo utakapofahamu kumcha BWANA, na kupata kujua Mungu.*"
- Mith. 1:7, "*Kumcha BWANA ni chanzo cha maarifa, bali wapumbavu hudharau hekima na adabu.*"

Ujuzi huo wa Mungu, ambayo ndiyo nyumba ya hekima na uelewa anawapa walio imara. Mith. 2:5-7, "*Ndipo utakapofahamu kumcha BWANA, na kupata kumjua Mungu. Kwa kuwa BWANA huwapa watu hekima; kinywani mwake hutoka maarifa na ufahamu; huwawekea wanyofu akiba ya hekima kamili; yeye ni ngao kwao waendao kwa ukamilifu.*"

Utataka Mungu akupatie kinga kuongoza maisha yako.

Yeye ni ngao kwa wale wanaotembea sahihi.

- Mith. 2:7, "*Huwawekea wanyofu akiba ya hekima kamili, yeye ni ngao kwao waendao kwa ukamilifu.*"
- Mith. 30:5, "*Kila neno la Mungu limehakikishwa; yeye ni ngao yao waaminio.*"

Anaongoza njia ya haki (ambayo wenye haki wanachukua).

- Mith. 2:8, "*Apataye kuyalinda mapito ya hukumu, na kuhifadhi njia za watakatifu wake.*"
- Zab. 23:3, "*Hunihuisha nafsi yangu; na kuniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake.*"

Anatunza njia za watakatifu wake.

- Mith. 2:8, "*Apate kuyalinda mapito ya hukumu, na kuhifadhi njia za watakatifu wake.*"
- Zab. 121:5-8, "*BWANA ndiye mlinzi wako; BWANA ni uvuli mkono wako wa kuume. Jua halitakupiga mchana, wala mwezi wakati wa usiku. BWANA atakulinda na mabaya yote, atakulinda nafsi yako. BWANA atakulinda utokapo na uingiapo, tangu sasa na hata milele.*"

Ni baraka iliyoje kupita katika maisha na Mungu akiwa upande wako!

Kuwa na maadili mema katika kuishi.

Utakuwa na uelewa mkuu.

Ya utauwa na haki. Mith. 2:9, "*Ndipo utakapofahamu haki na hukumu, na adili na kila njia njema.*"

Ya haki (pasipo upendeleo) na njia nzuri sana. Mith. 2:9, "*Ndipo utakapofahamu haki na hukumu, na adili, na kila njia njema.*"

Maombi ya Daudi, Zaburi 143:8-10, "*Unifanye kusikia fadhili zako asubuhi, kwa maana nimekutumaini wewe. Unijulishe njia nitakayoiendea, kwa maana nakuinulia nafsi yangu. Ee BWANA uniponye na adui zangu; nimekukimbilia wewe unifiche. Unifundishe kuyatenda mapenzi yako, kwa maana ndiwe Mungu wangu; Roho yako mwema aniongoze kwenye nchi sawa,*"

Utakuwa na mabadiliko...

Baada ya hekima kuingia katika moyo wako na ufahamu ikikupendeza wewe.

Mith. 2:10, "*Maana hekima itaingia moyoni mwako, na maarifa yatakupendeza nafsi yako;*"

Vitakutunza na kukuweka salama.

- Mith. 2:11, "*Busara itakulinda; ufahamu utakuhifadhi.*"
- Mith. 6:22-23, "*Uendapo yatakuongoza, ulalapo yatakulinda, na uamkapo yatazungumza nawe. Maana maagizo hayo ni taa, na sheria hiyo ni nuru, na maonyo ya kumwadilisha mtu ni njia ya uzima.*"

Ni baraka ya aina gani kuendelea katika maisha na hekima ya Mungu ikiwa upande wako!

Kutolewa katika watu wabaya.

Wanenao mambo makuu (machafu).

- Mith. 2:12, "*Ili kuokoka na njia ya uovu, na watu wanenao yaliyopotoka;*"
- Mdo. 20:30, "*Tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotofu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.*"

Waachao njia sahihi, na kutembea katika njia za giza.

- Mith. 2:13, "*Watu waziachao njia za unyofu, ili kuziendea njia za giza;*"

- 2 Pet. 2:20-22, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*"

Wafurahio katika kutenda uovu, wakifurahi katika upotovu wa waovu.

- Mith. 2:14, "*Wafurahio kutenda mabaya; wapendezwao na upotoe wa waovu;*"
- Mith. 10:23, "*Kwa mpumbavu kutenda maovu ni kama mchezo, bali mtu mwenye ufahamu ana hekima.*"

Waliopotoka katika njia zao, na wakaidi katika mapito yao.

- Mith. 2:15, "*Waliopotoka katika njia zao; walio wakaidi katika mapito yao.*"
- Mith. 1:10-19, "*Mwanangu mwenye dhambi wakikushawishi, wewe usikubali. Wakisema haya njoo pamoja nasi, na tuvizie ili kuwaga damu tumwotee asiye na hatia, bila sababu; tuwameze hai kama kuzimu, na wazima kama wao washukao shimoni. Tutapata mali yote ya dhamani, tutazijaza nyumba zetu mateka. Wewe utashirikiana nasi; tutakuwa na vitu vyote shirika. Mwanangu usiende njiani pamoja nao; uzuie mguu wako usiende katika mapito yao. Maana miguu yao huenda mbio maovuni, na hufanya haraka ili kumwaga damu. Kwa kuwa mtego hutegwa bure, mbele ya macho ya ndege ye yote. Na hao hujiotea damu yao wenyewe, hujinyemelea nafsi zao wenyewe. Ndivyo zilivyo njia za kila mwenye tama ya mali; huuondoa uhai wao walio nayo.*"

Kuokolewa kutoka katika wanawake waovu.

Mwenye kubembeleza kwa maneno yake malaini.

- Mith. 2:16, "*Ili kuokoka na mlaya, naam, Malaya mwenye kubembeleza kwa maneno yake;*"
- Mith. 7:5-21, "*Wapate kukulinda na Malaya, na mgeni akubembelezaye kwa maneno yake. Maana katika dirisha la nyumba yangu nalichungulia katika shubaka yake; nikaona katikati ya wajinga, nikamtambua miongoni mwa vijana, kijana*

mmoja asiyekuwa na akili, akipita njiani karibu na pembe yake, akiishika njia iendayo nyumbani kwake, wakati wa magharibi, wakati wa jioni, usiku wa manane gizani. Na tazama, mwanamke akamkuta, ana mavazi ya kikahaba, mwerevu wa moyo; ana kelele na ukaidi; miguu yake haikai nyumbani mwake. Mara yu katika njia kuu, mara viwanjani, naye huotea katika pembe za kila njia. Basi akamshika akambusu, akamwambia kwa uso usio na haya, kwangu ziko sadaka za amani; leo hivi nimeziondoa nadhiri zangu; ndiyo maana nikatoka nikulaki, nikutafute uso wako kwa bidii, nami nimekuona. Nimetandika kitanda changu magodoro mazuri, kwa matandiko ya Kimisri yenye mistari. Nimetia kitanda changu manukato, manemane na udi na mdalasini. Haya na tushibe upendo hata asubuhi, tujifurahishe nafsi zetu kwa mahaba. Maana mume wangu hayumo nyumbani, amekwenda safari ya mbali; amechukua mfuko wa fedha mkononi, atarudi wakati wa mwezi mpevu. Kwa maneno yake mengi na ulaini akamshawishi, kwa ubembelezi wa midomo yake akamshinda."

Mzinzi amwachaye mume wake na agano na Mungu.

- Mith. 2:17, "*Amwachaye rafiki wa ujana wake, na kulisahau agano la Mungu wake.*"
- Mal. 2:14, "*Lakini ninyi mwasema ni kwa sababu gani? Ni kwa sababu BWANA amekuwa shahidi kati yaw ewe na mke wa ujana wako, uliyemtenda mambo ya hiana, angawa yeye ni mwenzako, na mke wa agano lako.*"

Ambaye nyumba na njia zake uongoza katika kifo, na sehemu ambayo mtu harudi.

- Mith. 2:18-19, "*Maana nyumba yake inaelekea mauti, na mapito yake yanakwenda kwenye wafu. Katika hao wamwendeao harudi hata mmoja, wala hawazifikilii njia za uzima.*"
- Mith. 9:13-18, "*Mwanamke mpumbavu hupiga kelele, ni mjinga hajui kitu. Hukaa mlangoni pa nyumba yake, juu ya kiti mahali pa mjini palipoinuka, apate kuwaita wapitao njiani, waendao moja kwa moja katika njia zao. Kila aliye mjinga na aingie humu. Tena amwambia mtu aliyepungukiwa na akili, maji yaliyoibiwa ni matamu, na mkate ulioliwa kwa siri hupendeza. Lakini huyo hajui ya kuwa wafu wamo humo; ya kuwa wageni wake wamo chini kuzimuni.*

Hekima inaweza kutuondoa katika wanawake waovu na njia za maangamizi yao!

Kuwezeshwa kuishi maisha ya haki.

Kutembea katika njia nzuri na kukuweka katika mapito ya haki.

- Mith. 2:20, "*Ila upate kwenda katika njia ya watu walio wema, na kuyashika mapito ya wenye haki.*"
- Zab. 23:3, "*Huniuhisha nafsi yangu, na kuniongoza katika njia ya haki kwa ajili ya jina lake.*"
- Zab. 23:6, "*Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele.*"

Kuwa mwena na asiye na mawaa, kuishi na kubaki katika nchi.

- Mith. 2:21, "*Maana wanyofu watakaa katika nchi, na wakamilifu watadumu ndani yake.*"
- Zab. 37:3, "*Umtumaini BWANA ukatende mema, ukae katika nchi, upendezwe na uaminifu.*"

Kama ilivyo kwa waovu na wasio waaminifu, wakikatwa na kung'olewa katika nchi.

- Mith. 2:22, "*Bali waovu watatengwa na nchi, nao wafanyao hila watang'olewa.*"
- Zab. 37:37-38, "*Umwangalie sana mtu mkamilifu, umtazame mtu mnyofu, maana mwisho wake mtu huyo ni amani. Wakosaji wataangamizwa pamoja na wasio haki mwisho wao wataharibiwa.*"

Hekima inaweza kututia nguvu ili tuishi katika baraka zaidi, kama siyo kwa muda mrefu tunapoishi katika dunia hii!

Hitimisho

Je faida za hekima sio bora kuliko jitihada za kuipata?

- Kumjua Mungu na kufurahia ulinzi wake?
- Kupata ujuzi wa kufanya chaguzi sahihi?
- Kutolewa katika njia mbovu za watu waovu?
- Kutolewa katika kubembelezwa kwa wanawake waovu?
- Kuweza kutembea katika haki na amani, tukiishi maisha yaliobarikiwa na Mungu?

Je ni juhudi gani zinazohitajika ili kuwa na hekima ya Mungu?

- Kusikia neno la Mungu ("*utege sikio kusikiliza hekima*").
- Kukaa katika neno la Mungu ("*weka moyo wako katika kuelewa*").
- Omba kwa imani katika hekima ("*lia upate uelewa…inua sauti yako ili uelewe*").
- Kuthamini ubora wake kwa hali ya juu ("*uitafute kama fedha…kama hazina iliyofichwa*").

Kwa nguvu hizo, mtu hatapata tuu hekima kwa kila siku, maisha ya matendo, bali pia atampata Yesu Kristo. Kol. 2:3, "*Ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika.*" Hakika yeye ndiye faida kuu ya kutafuta hekima kwa bidii!